

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA KILIMO**  
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**



Telephone: (023) 2333303  
Fax: (023) 2333536  
E-Mail: [info@cashew.go.tz](mailto:info@cashew.go.tz)  
[www.cashew.go.tz](http://www.cashew.go.tz)  
Tarehe: 9 Oktoba, 2023

Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu  
Bodi ya Korosho Tanzania  
S.L.P. 533  
MTWARA

## **TANGAZO LA AJIRA ZA MUDA**

### **1. WASIMAMIZI WA USAFIRISHAJI BANDARINI MTWARA (NAFASI 20)**

#### **A. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA WASIMAMIZI WA USAFIRISHAJI BANDARINI**

- (a) Awe Mtanzania mwenye umri kati ya Miaka 18 - 40;
- (b) Awe amehitimu kidato cha IV na kufaulu masomo ya Kiswahili na Kiingereza;
- (c) Awe na Cheti cha Astashahada/ stashahada ya Manunuzi, Usafirishaji, Ugavi, Rasilimali Watu, Uhasibu, Biashara Masoko au sifa zinazofanana na hizo kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali
- (d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
- (e) Awe anaweza kusoma na kuandika vizuri katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili
- (f) Awe na Ngamizi Mpakato (**Laptop**).
- (g) Awe na uelewa wa kutumia Kompyuta.

#### **B. MAJUKUMU YA KAZI YA WASIMAMIZI WA USAFIRISHAJI BANDARINI**

- (a) Kupokea nyaraka za usafirishaji na kukagua kama zipo sahihi.
- (b) Kuhakiki uzito wa Korosho na magunia.
- (c) Kusimamia upakiaji wa Korosho (Stuffing).
- (d) Kufanya kazi kwa weledi kwa kushirikiana na TPA na TRA.
- (e) Kutunza taarifa zinazohusu upakiaji wa Korosho.

**Maombi yote yatumwe kwa anuani hii hapa chini kabla ya tarehe 15.10.2023 saa 10:00 jioni.**

MKURUGENZI MKUU,  
BODI YA KOROSHO TANZANIA,  
S.L.P 533,  
MTWARA

**Barua Pepe: [info@cashew.go.tz](mailto:info@cashew.go.tz)**

*'Cashewnut Board of Tanzania is an equal Opportunity Employer'*